JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA MKUU WA MKOA WA KATAVI

# MIAKA MINNE

## YA MHE. RAIS DKT. SAMIA SULUHU HASSAN



- Sekta ya Uchukuzi
- Sekta ya Afya
- Sekta ya Usafiri wa Anga








MARCH 2025



**Mhe. Mwanamvua Mrindoko**
Mkuu wa Mkoa wa Katavi

## 02. HALI YA MAENDELEO YA MKOA

**Mkoa** wa Katavi katika kipindi cha Miaka Minne ya Uongozi wa awamu ya sita ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan umepokea Jumla ya Shilingi **1,339,002,503,687.7 (Trilioni 1.339)** kwa ajili ya shughuli za kukuza uchumi, miradi mbalimbali ya maendeleo, kuboresha maisha na ustawi wa Jamii, utawala bora na uwajibikaji ndani ya Mkoa. Vilevile, fedha hizo ni kwa ajili ya kutekeleza Dira ya Taifa ya Maendeleo hadi 2025, Ilani ya Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2020, Mpango wa Taifa wa Maendeleo wa Miaka Mitano na Mikakati mbalimbali ya Serikali.

Mchanganuo wa Fedha zilizopokelewa Mkoani Katavi katika kipindi cha miaka minne ya uongozi wa Rais wa awamu ya sita Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan (2021/22, 2022//23, 2023/24 na 2024/2025)

***01)*** *Utekelezaji wa miradi Ofisi ya Mkuu wa Mkoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa*
***Tsh 384,882,734,945.50***

***02)*** *Hospitaliya Rufaa ya Mkoa* ***Tsh 18,189,133,604.19***

***03)*** *MUWASA*
***Tsh 32,163,080,399.89***

***04)*** *RUWASA*
***Tsh 33,529,634,479.08***

***05)*** *TANESCO*
***Tsh. 196,943,769,775.68***

***06)*** *TANROAD*
***Tsh 410,975,698,026.00***

***07)*** *TARURA*
***Tsh 63,943,451,708.12***

***08)*** *Ujenzi wa Bandari ya Karema*
***Tsh 47,974,892,364.00***

***09)*** *Miradi ya Umwangiliaji*
***Tsh 54,686,490,435.28***

***10)*** *Biashara ya Kaboni*
***Tsh 22,511,000,000.00***

***11)*** *Jengo Jipya la Abiria Uwanja wa Ndege*
***Tsh 1,444,617,687.63***

***12)*** *Mahakama*
***Tsh 8,300,000,000.00***

***13)*** *Polisi Mkoa*
***Tsh 800,000,000.00***

***14)*** *Ofisi ya Taifa ya Mashtaka* ***Tsh 1,403,548,703.00***

***15)*** *Ujenzi wa Vyuo viwili vya Veta* ***Tsh 649,388,484.02***

***16)*** *NFRA*
***Tsh 14,000,000,000.00***

***17)*** *Jengo Jipya la Utawala NAOT Katavi*
***Tsh 4,800,000,000.00***

***18)*** *Mradi wa usanifu na ujenzi wa Reli (Kaliua –Mpanda) wenye urefu wa njia ya reli kilomita 210.*
***Tsh 17,025,396,281.31***

***19)*** *TASAF*
***Tsh 7,319,666,794.00***

***20)*** *Ujenzi wa madarasa na Daaria Chuo Kikuu Sokoine Kampasi ya Mizengo Pinda*
***Tsh 17,460,000,000.00***

***Jumla***
***Tsh 1,339,002,503,687.7***

## 3. SEKTA YA ELIMU

Hadi kufikia Machi, 2025 Mkoa una jumla ya Shule za Msingi 293, ambapo kati ya hizo za Serikali ni 278 na zisizo za Serikali ni 15. Mkoa una Shule za Sekondari zipatazo 79 zikiwemo 74 za Serikali na 5 ni Shule za binafsi.





*Maendeleo ya Ujenzi wa Shule ya Sekondari ya Wavulana Katavi*

Kwa kipindi cha uongozi wa Rais wa awamu ya sita, Sekta ya Elimu imepokea kiasi cha **Shilingi 57,870,265,268.7 (Bilioni 57.870)** zilizotumika katika kuboresha miundombinu ya Shule mbalimbali na kuweka mazingira mazuri ya kufundishia na kujifunza pamoja na Ujenzi wa Shule mpya mia moja ishirini na tisa (129) zikiwemo Shule 97 za Msingi na Shule 32 za Sekondari, madarasa 689, madarasa ya awali 6, matundu ya vyoo 112. Hii imepunguza kwa kiasi kikubwa umbali wa kutembea kwenda Shule na msongamano wa Wanafunzi madarasani na kuwezesha mazingira bora zaidi kwa Walimu na Wanafunzi.

## Mchanganua wa Fedha za Miradi Sekta ya Elimu

**01. Serikali Kuu**
Madarasa 39, matundu 92 ya vyoo,Mabweni 3 na mabwalo 4.
Kiasi cha fedha kilichopokelewa ni Tsh. **1,967,529,000**

**02. GPE - Lanes**
Madarasa 6, Madarasa ya Awali 6, matundu 85 ya vyoo na ukarabati wa vituo vya walimu 6.
Kiasi cha fedha kilichopokelewa ni Tsh. **637,320,000**

**03. BOOST**
Shule Mpya 12, vyumba vya madarasa 171, Matundu ya Vyoo 172, Nyumba za Walimu 2, na Ukarabati wa Shule Kongwe 1.
Kiasi cha fedha kilichopokelewa ni Tsh. **11,347,800,000**

**04. SEQUIP**
Shule Mpya 15 ( Shule za kata 11, Shule za amali 2,Shule ya Wasichana Katavi na Shule ya Kanda ya Wavulana Katavi), ujenzi nyumba 11 za waalimu, Miundombinu ya Kidato cha Tano katika Shule (2) za Ikuba na Kawalyowa na matundo 20 ya vyoo. Kiasi cha fedha kilichopokelewa ni Tsh. **24,083,486,756.00**

**05. Miradi ya UVIKO-19**
madarasa **426.** Kiasi cha fedha kilichopokelewa ni Tsh. **8,523,744,759.84**

**06. EP4R**
Ujenzi wa Madarasa 47 na ukamilishaji madarasa (maboma) 76. Kiasi cha fedha kilichopokelewa ni Tsh. **1,891,890,183.35**

**07. BARRICK**
Upanuzi wa Shule zenye kidato cha tano na sita kwenye Shule za Sekondari Nsimbo (Mabweni 2 na matundu 8 ya vyoo), Usevya (Bweni 1, madarasa 3 na matundu 6 ya vyoo na Kabungu (Madarasa 5).
Kiasi cha fedha kilichopokelewa ni Tsh. **646,800,000.00**

**08. SERIKALI KUU**
Elimu bila ada. Kiasi cha fedha kilichopokelewa ni Tsh. **8,771,694,569.51**

Jumla Kuu ni Tsh **57,870,265,268.70**

## Miundombinu ya Shule Msingi

Katika kipindi cha Uongozi wa awamu ya sita miundombinu katika Shule za msingi imeongezeka kama ifuatavyo:-

- Idadi ya Shule za msingi imeongezeka kutoka Shule **196** mwaka 2021 hadi Shule **293** mwaka 2025 sawa na ongezeko
- Idadi ya madarasa imeongezeka kutoka madarasa **1,596** mwaka 2021 hadi madarasa **3,815** mwaka 2025 sawa na ongezeko la madarasa **2,219.**
- Idadi ya madawati imeongezeka kutoka madawati **20,079** mwaka 2021 hadi kufikia madawati **52,807** mwaka 2025 sawa na ongezeko la madawati **32,728.**
- Idadi ya matundu ya vyoo imeongezeka kutoka matundu ya vyoo **1,669** mwaka 2021 hadi kufikia matundu ya vyoo **4,403** sawa na ongezeko la matundu ya vyoo **2,734**.



*Shule ya Sekondari Mlele iliyopo Kata ya Inyonga, H/W ya Mlele*

• Idadi ya nyumba za walimu imeongezeka kutoka nyumba za walimu 604 mwaka 2021 hadi kufikia nyumba za walimu **678** mwaka 2025 sawa na ongezeko la nyumba 74 za Walimu.




*Jengo la Utawala la Shule ya Sekondari Mwese, iliyopo katika Kata ya Mwese, H/W ya Tanganyika.*

## Miundombinu ya Elimu Sekondari

Katika kipindi cha Uongozi wa Awamu ya sita miundombinu katika Shule za Sekondari umeongezeka kama ifuatavyo: -

• Idadi ya Shule za Sekondari imeongezeka kutoka Shule **47** mwaka 2021 hadi Shule **79** mwaka 2025 sawa na ongezeko la Shule **32**,

• Idadi ya madarasa imeongezeka kutoka madarasa **579** mwaka 2021 mpaka madarasa **1,138** kufika mwaka 2025 sawa na ongezeko la madarasa **559**,

• Idadi ya viti/meza imeongezeka kutoka viti/meza **21,514** mwaka 2021 hadi kufikia viti/meza **36,727** mwaka 2025 sawa na ongezeko la viti/meza **15,213**,

• Idadi ya matundu ya vyoo imeongezeka kutoka matundu ya vyoo **1,274** mwaka 2021 hadi kufikia matundu ya vyoo **3,421** mwaka 2025 sawa na ongezeko la matundu **2,147** ya vyoo.

• Idadi ya nyumba za walimu imeongezeka kutoka nyumba **191** mwaka 2021 hadi kufikia nyumba **225** mwaka 2025 sawa na ongezeko la nyumba **34.**

## Elimu ya Mafunzo ya Ufundi Stadi (VETA)

Mkoa unatekeleza miradi miwili (2) ya ujenzi wa vyuo vya VETA katika Halmashauri za Tanganyika na Mlele. Miradi yote inatekelezwa kwa gharama ya Shilingi **3,233,118,565.41 (Bilion 3.233),** Mpaka kufikia Machi, 2025 Mkoa umepokea jumla ya Shilingi **821,388,482.02.**
Kwa upande wa Halmashauri ya Wilaya ya Tanganyika utekelezaji wa mradi umefikia hatua ya boma sawa na 32.54% na Halmashauri ya Wilaya ya Mlele mradi upo hatua ya boma sawa na 33%. Miradi yote inatarajiwa kukamilika mwaka huu wa fedha 2024/2025.

# 04. SEKTA YA AFYA

Hadi kufikia Machi, 2025 Mkoa una jumla ya vituo 161 vinavyotoa huduma za afya. Kati ya vituo hivyo kuna Hospitali moja (1) ya Rufaa ya Mkoa, Hospitali tano (5) za Halmashauri, Vituo vya Afya 28 na Zahanati 127.

Mwaka 2021, Mkoa ulikuwa na jumla ya watumishi **898** na hadi kufikia Machi 2025, Mkoa una jumla ya watumishi **1,754**. Ikijumuisha na watumishi wapya 262 walioajiriwa na Serikali Mwezi Septemba – Desemba 2024 pamoja na watumishi **98** waliojiriwa kwa mikataba kwenye miradi mbalimbali ya Afya ambapo ni sawa na ongezeko la watumishi **856.**

**Mchanganuo wa Mapokezi ya fedha Sekta ya Afya (2021/2022-2024/25)**

01. Hospitali ya Rufaa ya Mkoa, Ujenzi/Ukarabati **Tsh. 18,386,053,967.189**

02. Hospitali 4 za Wilaya, Ujenzi/Ukarabati **Tsh. 10,370,000,000.00**

03. Miradi ya UVIKO 19 (ICU na EMD), Ujenzi/Ukarabati **Tsh. 1,200,000,000.00**

04. Miradi ya Tozo, Ujenzi/Ukarabati **Tsh 1,750,000,000.00**

05. Ukarabati wa Hospitali Kongwe (Mpanda MC) Ujenzi/Ukarabati **Tsh. 900,000,000.00**

06. Ukarabati na Ujenzi wa Zahanati 36 na Vituo vya Afya 20, Ujenzi/Ukarabati **Tsh. 6,721,961,459.59**

07. Vifaa tiba vya Hospitali, Ujenzi/Ukarabati **Tsh. 1,200,000,000.00**

08. Vifaa tiba vya vituo vya Afya, Ujenzi/Ukarabati **Tsh. 600,000,000.00**

09. Vifaa tiba vya Zahanati, Ujenzi/Ukarabati **Tsh. 500,000,000.00**

Jumla Kuu, **Tsh 41,628,015,426.779**



*Rais wa JMT, Mhe. Rais Dkt. Samia Suluhu akimsikiliza Dkt. Maria Matei katika wodi ya watoto njiti (NICU) katika Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Katavi (Julai 14, 2024)*




*Kituo cha Afya Sibwesa kilichopo Kata ya Sibwesa Tarafa ya Mwese, H/W ya Tanganyika.*

## Vituo vya kutolea huduma za Afya

Mkoa wa Katavi umeendelea kutekeleza Mpango wa Maendeleo ya Afya ya Msingi (MMAM) ambapo Mwaka 2021 Mkoa ulikuwa na jumla ya vituo **102** vya kutolea huduma za Afya na hadi kufikia Mwezi Machi, 2025 Mkoa una Jumla ya vituo vya kutolea huduma za Afya **161** ikiwa ni ongezeko la vituo **59**, Sawa na ongezeko la asilimia **36.64.**

I. Zahanati zimeongezeka kutoka **80** mwaka 2021 hadi 127 mwaka 2025 sawa na ongezeko la zahanati **47**

II. Vituo vya Afya vimeongezeka kutoka **17** mwaka 2021 hadi kufikia **28** mwaka 2025 sawa na ongezeko la vituo **11** sawa na ongezeko la asilimia **39**

III. Ukamilishaji wa Hospitali **4** za Wilaya na ukarabati wa hospitali Kongwe ya Manispa ya Mpanda umekamilika.

## Hospitali ya Rufaa ya Mkoa

Kwa upande wa Hospitali ya Rufaa ya Mkoa fedha **Bilioni 18.386** zilizopokelewa kwa kipindi cha miaka minne zimesaidia kukamilisha;

- Miundombinu ya jengo la 'Wing A" lenye huduma za wagonjwa wa nje, huduma za mama na mtoto, Vipimo vya radiologia na vyumba vya upasuaji.

- Ujenzi wa jengo la 'Dialysis" (Huduma ya kusafisha Damu) umekamilika kwa asilimia 100 na huduma zimeanza kutolewa.

- Ujenzi wa jengo la huduma za dharura (EMD), Ujenzi wa jengo la wagonjwa mahututi (ICU), Ujenzi wa nyumba ya mtumishi.

- Ununuzi wa mashine ya CT-Scan, Ununuzi wa mashine mbili za kisasa za mionzi (digital X-Ray) pamoja na Ununuzi wa Vifaa tiba mbalimbali.

Mafanikio makubwa ya Hospitali ya Rufaa ya Mkoa ni wananchi kupata huduma kirahisi, kupunguza kusafirisha wagonjwa kwenda nje kwa kuendelea kupata huduma za ki-bingwa ambazo ni Huduma za kibigwa za upasuaji, Huduma za kibingwa za mifupa, Huduma za kibingwa za afya ya uzazi, Huduma za kibingwa za sikio, pua na kinywa, huduma za




*Jengo la 'Dialysis" (Huduma ya kusafisha Damu) Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Katavi*

kibingwa za Magonjwa ya Ndani pamoja na huduma za kibingwa za magonjwa ya dharura.

## Hali ya Upatikanaji wa Dawa na Vifaa Tiba

Mwaka 2021 Mkoa ulipokea kiasi cha Tshs **2,980,556,000.00** za ununuzi wa dawa, Vifaa, Vifaa tiba na vitendanishi na kwa mwaka 2024 mkoa umepokea kiasi cha Tshs **3,380,560,000.00** Kumekuwa na ongezeko la bajeti ya dawa kwa kiasi Tshs **400,000,000.00** sawa na asilimia 11.8.

Hadi kufikia mwezi Machi 2025 wastani wa upatikanaji wa dawa ni asilimia 89

## Huduma za Dharura kwa kina Mama Wajawazito na Watoto Wachanga (CEmONC)

kumekuwa na ongezeko la vituo vilivyoboreshwa vyenye uwezo wa kutoa huduma za dharura ikiwa ni pamoja na huduma za upasuaji kwa kina mama wajawazito kutoka vituo **8** Mwaka 2021 hadi kufikia vituo **14** Mwaka 2025.
Aidha, Wajawazito wanaojifungulia kwenye vituo vya huduma wameongezeka mwaka hadi mwaka Kina mama **40,269** mwaka 2021 hadi kufikia kina mama **48,322** mwaka 2025.

## Magari ya Wagonjwa

Kumekuwa na ongezeko la magari ya wagonjwa (Ambulance) kutoka **10** mwaka 2021 hadi **17** mwaka 2025, Magari haya yamerahisisha usafirishaji wa Wagonjwa wanaohitaji huduma za rufaa kutoka ngazi ya Zahanati na Vituo vya Afya Kwenda Hospitali za Wilaya pamoja na Hospitali ya Rufaa ya Mkoa.

# 05. SEKTA YA MAJI

**Mamlaka ya Maji na Usafi wa Mazingira Mpanda (MUWASA).**

Mamlaka ya Maji na Usafi wa Mazingira Mpanda (MUWASA) inatoa huduma ya Maji katika Kata 15 za Manispaa ya Mpanda. Mahitaji ya Maji ni lita **Milioni 15,974,660** kwa siku. Mamlaka ina uwezo wa kusambaza mahitaji ya Maji kwa asilimia 39.22 kwa siku.

Katika kipindi cha uongozi wa Rais wa awamu ya Sita, Mkoa umeendelea kutekeleza miradi minne yenye thamani ya Shilingi bilioni **32,163,080,399.89** ambayo ikikamilika itaongeza upatikanaji wa Maji kwa zaidi ya asilimia 100.
Ndugu Wananchi, Mkoa unaendelea kutekeleza mradi wa usamabazaji Maji kutoka Bwawa la Milala unaotekelezwa chini ya mpango wa ujenzi wa mradi wa Maji wa Miji 28. Mradi huu unatarajiwa kuzalisha Maji lita **12,000,000** kwa siku na kunufaisha wakazi wote wa Manispaa ya Mpanda. Hadi kufikia Machi, 2025 hatua ya utekelezaji imefikia asilimia 38 mradi unatekelezwa kwa muda wa miezi 30 kuanzia 11 Aprili, 2023 na unatarajiwa kukamilika Mwezi Oktoba 2025.

**Wakala wa Usambazaji Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini (RUWASA)**

kwa upande wa Maji Vijijini katika kipindi cha uongozi wa Rais wa awamu ya Sita, Mkoa kupitia RUWASA umepokea jumla ya Tsh. **33,529,634,479.08 (Bilioni 33.352)** kwa ajili ya miradi 51 ya Maji vijijini. Utekelezaji wa miradi hii imesaidia kuongeza idadi ya watumiaji wa Maji vijijini kutoka asilimia 62.2 mwaka 2021 hadi kufikia asilimia 77.3 Machi, 2025 sawa na ongezeko la asilimia 15.1




*Tenki la Maji lenye ujazo wa lita 100,000 lililopo katika Kata ya Kanoge, H/W ya Nsimbo*

# 06. SEKTA YA UMEME

Mkoa wa Katavi pamoja na Wilaya zake zinapata Umeme unaofuliwa katika vituo viwili (2) vilivyopo Mpanda Mjini (MW 7.5) na Mlele (MW 1.44) ambavyo vinatumia mafuta mazito ya dizeli. Halmashauri ya Mpimbwe inapokea Umeme kutokea Sumbawanga ambao ni wa gridi ya Taifa ya Zambia eneo la Mbala.

## Mapokezi ya fedha Sekta ya nishati ya Umeme (2021/2022-2024/25)

Katika kipindi cha uongozi wa Rais wa awamu Mkoa umepokea jumla ya Shilingi **196,402,687,825.08 (Bilioni 196.4)** kwa ajili ya utekelezaji wa miradi mbalimbali ya Umeme ikiwemo Upanuzi wa mtandao wa Umeme kwa Wilaya ya Mpanda, Tanganyika na



*Mkuu wa Wilaya ya Mlele Mhe. Majid Mwanga akikagua Mradi wa kusafirisha umeme kutoka Tabora hadi Katavi unaotekelezwa na Kampuni ya Ujenzi na Ukarabati wa Miundombinu na Usambazaji wa Umeme nchini ( ETDCO).*



*Wafanyakazi wa Kampuni ya Ujenzi na Ukarabati wa Miundombinu ya Usafirishaji na Usambazaji Umeme (ETDCO) wakiwa kazini wakitekeleza mradi wa ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme kutoka Mkoa wa Tabora hadi Katavi.*

*Inatoka UK wa 08*

Mlele, Kuongeza nguvu ya Umeme (Voltage improvement) kwa Wilaya ya Mpanda, Tanganyika na Mlele, kupeleka Umeme kwenye Vijiji kwa ufadhili wa REA awamu ya kwanza katika Vijiji vyote **172** vya Mkoa na vina Umeme. Upelekaji wa huduma hizi umeongeza idadi ya wateja wanao tumia Umeme kutoka wateja **23,312** mwaka 2020/21 hadi wateja **42,567** Machi, 2025 na kumeleta chachu ya ongezeko la mapato kutoka shilingi **494,496,385.22** hadi shilingi **1,031,280,772.87** kwa mwezi.

## Ujenzi wa Mradi wa Grid ya Taifa

Mkoa wa Katavi unategemea kupata Umeme kupitia mradi mkubwa wa Gridi ya Taifa wenye thamani ya shilingi billion 116 kutokea Tabora 132KV. Ujenzi wa njia kubwa ya Umeme ya msongo wa Kilovoti 132 kutoka Tabora hadi Katavi umbali wa kilomita 383 na kujenga vituo vya kupoozea Umeme katika eneo la Inyonga chenye ukubwa wa 12MW na eneo la Mpanda chenye ukubwa wa 28MW. Utekelezaji wa mradi huu hadi Machi, 2025, umefikia asilimia 94 na pindi utakapokamilika kwa mara ya kwanza Mkoa wa Katavi utakuwa umeunganishwa na Umeme wa Grid ya Taifa.

## Fedha za Miradi ya Maendeleo kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025.

Katika mwaka wa fedha TANESCO Mkoa wa Katavi uliidhinishiwa kutumia kiasi cha shilingi **10,838,286,911.00** kwa ajili ya miradi ya kuboresha huduma ya Umeme kwa mchanganuo ufuatao:

- Miradi 17 ya matengenezo ya miundombinu (Repair and Maintenance) yenyenye gharama ya kisai cha shilingi **2,074,626,028.00**

- Miradi 31 ya uboreshaji wa nguvu ya Umeme (Voltage Improvement Project) yenyenye gharama ya kisai cha shilingi **2,809,989,880.00**

- Miradi 25 mipya ya usambazaji wa Umeme (New extension Projects) yenyenye gharama ya kisai cha shilingi **2,223,777,753.00**

- Mradi wa usambazaji Umeme kwenye Vitongoji 75 vya Mkoa wa Katavi kwa kila jimbo vitongoji 25 kwa gharama ya shilingi **9,541,080,476.44.** Mradi utakamilika tarehe **04.09.2026**, hatua ya mradi ipo kwenye usanifu na ununuzi wa vifaa.



*Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, Mhe. Doto Biteko akipata maelezo ya kitaalamu kuhusu mradi wa njia ya kusafirisha umeme kutoka Tabora hadi Mpanda pamoja na ujenzi wa kituo cha kupokea, kupoza na kusambaza umeme cha Inyonga, Mlele Katavi.*

# 07. SEKTA YA MIUNDOMBINU YA BARABARA

## Wakala wa Barabara Mkoa (TANROADS)

Wakala ya Barabara (TANROADS) Mkoa anahudumia mtandao wa barabara wenye jumla ya kilometa **1,201.81**. Kati ya hizo kilomita **594.46** ni barabara kuu na kilomita **607.35** ni barabara za mikoa. Wananchi wa Mkoa wa Katavi wanashukuru kwa kuwajenga barabara ya Mpanda – Tabora yenye Kilometa **352** ambayo imekuwa ni chachu kubwa ya ukuaji wa uchumi wa wananchi kupitia sekta ya usafiri na usafirishaji na kuufungua Mkoa wa Katavi kwa fursa mbalimbali.

Mkoa wa Katavi unapongeza juhudi za Serikali chini ya uongozi wa Rais wa awamu ya Sita kwa kuleta kiasi cha shilingi **billioni 410,975,698,026.00** kwa ajili ya miradi ya kimkakati na ya kitaifa. Miradi hii itakapokamilika mtandao wa barabara kwa kiwango cha lami utaongezeka kutoka kilomita **325.81** na kufikia kilomita **548.45.**

Katika mwaka wa fedha 2023/24 Mkoa wa Katavi ulitekeleza miradi 39 yenye jumla ya Shilingi bilioni **15.092** kwa ajili ya kufanya matengenezo ya Barabara kuu na za Mkoa zenye jumla ya kilomita **1,201.81** pamoja na Kufanya matengenezo ya kinga katika madaraja na kujenga madaraja mapya.

## Miradi ya Kimkakati na ya Kitaifa Inayotekelezwa Mkoani Katavi

Mkoa wa Katavi unatekeleza miradi 7 ya kitaifa yenye jumla ya Shilingi **bilioni 405,313,485,100.00** kama ifuatavyo: -

- Barabara ya Mpanda - Uvinza - Kanyani (km 250.44) sehemu ya 2: Vikonge – Luhafwe (km 25) kwa gharama ya kiasi cha shilingi **35,638,514,918.00**

- Barabara ya Mpanda - Uvinza - Kanyani (km 250.44) sehemu ya 3: luhafwe - Mishamo



*Barabara yenye kiwango cha lami Katavi - Tabora*

*Inatoka UK wa 11*

/Bulamata jct (km 37.35) gharama ya mradi ni kiasi cha shilingi **58,629,442,494.00**

• Barabara ya Kibaoni – Sitalike sehemu ya 1: Kibaoni – Mlele jct (50 km) gharama ya mradi ni kiasi cha shilingi **88,725,676,540.00,**

• Barabara ya Kagwira – Karema 110.29 km sehemu ya 1: Kagwira - Kasekese (54.146 km) gharama ya mradi ni kiasi cha shilingi **106,947,754,011.00,**

• Barabara ya Kagwira – Karema sehemu ya 2: Kasekese – Karema port (56.144 km) gharama ya mradi ni shilingi **112,141,534,137.00**,

• Ujenzi wa kitanda cha daraja la Kavuu (urefu wa mita 87.5) gharama ya mradi ni shilingi **1,443,100,000.00** na

• Ujenzi wa daraja jipya la mto lugufu (urefu wa mita 42) gharama ya mradi ni Tsh. **1,787,463,000.00**

## Miradi ya Kimkakati inayofadhiliwa na Benki ya Dunia (CERC) Mkoani Katavi

Aidha ofisi ya Wakala ya Barabara Mkoa wa Katavi umefanikiwa kupata miradi 3 ya madaraja ambayo inafadhiliwa na Benki ya Dunia yenye jumla ya kiasi cha shilingi **17,286,798,663.5.**

Miradi hiyo ni kama ifuatavyo;

Ujenzi wa Daraja la Katuma/Sitalike kwa gharama ya Tsh. **9,106,208,961.00,**

Ujenzi wa Daraja la Mirumba/Kitumba kwa gharama ya **Tsh 6,399,538,440.00** na

Ujenzi wa Daraja la Kilida kwa gharama ya Tsh. **1,781,051,262.50.**



## Wakala wa Barabara za Vijijini na Mijini (TARURA)

Wakala wa Barabara za Vijijini na Mijini (TARURA) unahudumia mtandao wa barabara wenye jumla ya urefu wa kilomita 2,796.254 ambapo kati ya hizo kilomita 38.141 ni za Lami, kilomita 519.749 ni changarawe na kilomita 2238.364 ni za udongo.

## Mapokezi ya fedha TARURA Kwa (2021/2022-2024/25)

Katika kipindi cha miaka minne chini ya uongozi wa Rais wa awamu ya Sita, Mkoa umepokea kiasi cha Tsh. **63,943,451,708.12** (Bilioni 63.94)



*Daraja la Mto Mwali linalounganisha Vijiji vya Nyagantambo, Bungwe na Ifinsi.*

*Inatoka UK wa 12*

kwa ajili ya ujenzi wa barabara yenye urefu wa kilometa 17.6 kwa kiwango cha lami, Kilometa 475 za kiwango cha Changarawe, kufungua barabara mpya zenye urefu wa Kilometa 487, ujenzi wa madaraja ya kati (Box Kalavati) 31, ujenzi wa makalavati ya kawaida 672 na ujenzi wa madaraja ya mawe 20.

## Mpango wa Kazi za Barabara mwaka wa fedha 2024/2025

Katika Bajeti ya Mwaka wa fedha 2024/2025, TARURA Mkoa wa Katavi iliidhinishiwa jumla ya **Shilingi 13,990,596,716.52** kwa ajili ya matengenezo ya barabara, madaraja na usimamizi kwa mchanganuo ufuatao:-

Fedha za matengenezo ya barabara (Mfuko wa Barabara) ni **Shilingi 4,136,093,238.26** Fedha za Tozo **6,354,500,000.00** Fedha za Serikali Kuu (Jimbo) **Shilingi 2,500,000,000.00** Fedha za maendeleo kutoka mfuko wa Barabara **Tsh 1,000,000,000.00**

## Kazi zilizopangwa kufanyika kwa mwaka wa fedha 2024/2025

Kazi zilizopangwa kufanyika katika mwaka wa fedha 2024/2025 kwenye Halmashauri zote tano (5) za Mkoa wa Katavi ni pamoja na kufanya Matengenezo ya jumla ya Km 226.145 ambapo kati ya hizo Km 4.5 zitajengwa kwa kiwango cha Lami, Km 79.78 changarawe na Km 141. 865 zitajengwa kwa kiwango cha udongo, Ujenzi wa Kalvati 153, madaraja ya upinde wa mawe 4, Boksi Kalavati 33, mifereji mita 8,617 na Kufunga taa 46 za barabarani.

Katika mwaka wa fedha 2024/2025, TARURA Mkoa wa Katavi ulipanga kutekeleza kazi za Barabara kupitia Mikataba 32.
Hadi sasa, Jumla ya mikataba 27 imetangazwa na imeshapata Makandarasi.

# 08. BANDARI YA KAREMA

Mradi wa ujenzi wa Bandari ya Karema katika mwambao wa Ziwa Tanganyika wenye gharama ya Tsh **47,974,892,364.00 (Bilioni 47.97)** umekamilika na unatumika.

Bandari hii imerahisisha usafirishaji wa abiria na mizigo ambao umeboresha kufanyika kwa biashara baina ya Tanzania na nchi jirani za Congo DRC, Rwanda, Zambia na Burundi na kukuza uchumi wa Mkoa wa Katavi na Nchi kwa ujumla.




*Tenki la Maji lenye ujazo wa lita 100,000 lililopo katika Kata ya Kanoge, H/W ya Nsimbo.*





*Ziara ya Naibu Waziri wa Uchukuzi Mhe. David Kihenzile alipotembelea Bandari ya Karema iliyojengwa kwa gharama ya Tsh. Bilioni 47.97*

# 09. SEKTA YA USAFIRI WA ANGA

Mkoa una huduma ya uhakika ya usafiri wa anga kati ya Mpanda na Dar - Es- Salaam ambao unafanywa mara tatu (3) Siku za Jumatatu, Alhamisi na Jumamosi kwa wiki kupitia Shirika la Ndege la Tanzania (ATC). Uwepo wa uhakika wa safari za ndege kupitia shirika hili, unarahisisha kwa kiwango kikubwa mawasiliano na kuimarisha Shughuli za kiuchumi na kijamii kwa wananchi wa Mkoa wa Katavi. Mkoa umepokea Shilingi 1,444,617,687.63 (Bilioni 1.444) kwa ajili ya kuendelea na maboresho ya Uwanja wa Ndege Mpanda katika ujenzi wa jengo la utawala.



*Jengo jipya la abiria uwanja wa ndege Mpanda*






*Ziara ya Naibu Waziri wa Uchukuzi Mhe. David Kihenzile alipotembelea jengo jipya la abiria lililojengwa kwa gharama ya Tsh. Bilioni 1.44*

# 10. UKUSANYAJI WA MAPATO YA SERIKALI

Kwa kipindi cha miaka minne cha awamu ya sita ya Mkoa wa Katavi umekusanya jumla ya kiasi cha Tsh **118,526,664,138.81** (Bilioni 118.5). Kati ya makusanyo hayo, Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) imekusanya kiasi cha Tsh **28,448,421,591.64,** Mamlaka za Serikali za Mitaa kiasi cha shilingi **70,878,242,547.17** na makusanyo ya uuzaji wa madini kiasi cha shilingi **27,462,795,545.82.**

Hii ni kutokana na mazingira mazuri yaliyowekwa na Serikali ya Awamu ya Sita kwa Wafanyabiashara katika Mkoa wa Katavi.



*Dhahabu*

# 11. SEKTA YA KILIMO, MIFUGO NA UVUVI

Sekta hii inachangia asilimia 90 ya pato la Mkoa na inaajiri kwa asilimia 85. Ardhi inayofaa kwa kilimo ni hekta **932,136**. Eneo linalofaa kwa umwagiliaji ni jumla ya hekta **124,761**.

Mazao yanayolimwa ni pamoja na Tumbaku, Pamba, Alizeti, Korosho, Chikichi, Ufuta, Karanga, Mahindi, Mpunga, Mihogo, maharage, Viazi vitamu na Ndizi.
Mkoa unavuna mazao na kubaki na ziada.



*Zao la Mahindi*



*Mifugo*

Hadi sasa katika msimu wa mavuno 2023/2024 Mkoa umezalisha jumla ya Tani **1,410,877** zikiwemo Tani **1,330,165** za mazao ya chakula, Tani **71,619** za mazao ya biashara na Tani **9,094** za mazao ya bustani. Mahitaji ya Mkoa ya chakula kwa mwaka 2024/25 ni Tani **1,330,165.** Hii inafanya kuwa na ziada ya Tani **855,385**. Ongezeko la uzalishaji wa mazao limechochewa na matumizi ya mbolea za ruzuku, maboresho ya barabara, reli, bandari, masoko na kujituma kwa wananchi na hali ya hewa nzuri.

matumizi ya mbolea yameongezeka kutoka tani **10,104** hadi tani **13,189** na mbegu kutoka tani **4,851** hadi tani **5,263.50** mwaka 2022/23 na mwaka 2023/24 mtawalia.

Matumizi ya zana bora yameongezeka (matrekta makubwa yameongezeka kutoka **169** hadi **173** mashine za kuvunia mpunga (Combine harvester) kutoka **4** hadi **8** na matrekta madogo kutoka **207** hadi **281**. Aidha, matumizi ya zana bora za kilimo yameongezeka kutoka asilimia 14 hadi kufikia asilimia 30 mwaka 2022/23 na mwaka 2023/24 mtawalia.

Katika msimu wa kilimo wa 2024/2025 Mkoa umelenga kulima jumla ya hekta **390,128** zikiwemo hekta **317,696** za mazao ya chakula na hekta **85,621** za mazao ya biashara na kuzalisha jumla ya tani **1,434,149** zikiwemo tani **1,337,021** za mazao ya chakula na tani **97,128** za mazao ya biashara

Hali ya utekelezaji wa Mpango wa Mbolea za Ruzuku, 2023/24.
Mikoa iliyonufaika kwa kiasi kikubwa na mbolea za Ruzuku ambapo Zaidi ya tani 6,905 zenye thamani ya shilingi **4,467,349,922** za mbolea zenye Ruzuku zimeweza kusambazwa na kutumiwa na wakulima.
Wakulima wapatao **73,073** wameweza kusajiliwa na wakulima wapatao **26,534** wameweza kunufaika na mbolea za ruzuku Mkoani Katavi.

# 12. MALIASILI (BIASHARA YA KABONI)

Utunzaji wa Mazingira, Misitu na vyanzo vya Maji, umewezesha Mkoa kuingia kwenye biashara ya Kaboni (hewa Ukaa) katika Halmashauri ya Wilaya ya Tanganyika ambapo hadi sasa Mkoa umefanikiwa kupata mapato jumla ya Shilingi **22,511,000,000.00** fedha za Kitanzania na kufanikiwa kujenga Madarasa 52, Kukarabati Madarasa 20, ujenzi wa nyumba 5 (2 kwa 1), ujenzi wa nyumba 1 (3 kwa 1), ujenzi wa vichomea taka 6 (Incenerators), ujenzi wa mashimo 6 ya ya kondo la Mama (Placenta pits) kwenye vituo vya kutolea huduma za Afya, ukamilishaji wa Zahanati 1, ujenzi wa matundu **128** ya vyoo, utengenezaji wa madawati **1,496**, ujenzi wa Ofisi za vijiji 8, ujenzi wa Masoko 2 ya vijiji 2, ajira 112 kwa Vijana wanaolinda Misitu, utoaji wa kadi za Bima ya Jamii – CHF iliyoboreshwa (iCHF) za Afya kwa kaya **4,400**, Ajira za walimu 20 wa mikataba, Utoaji wa chakula cha wanafunzi kwenye Shule **16** na utoaji wa mikopo yenye thamani ya **shilingi 117,213,800.00** kwa Wanawake wajasiriamali.

Aidha kupitia fedha **bilioni 14,255,000,000** za biashara ya kaboni zilizopokelewa hivi karibuni Mkoa kwa kushirikiana na Halmashauri ya Wilaya ya Tanganyika umepanga kuendelea Kujenga na kukarabati miundombinu ya Shule za Msingi na Sekondari, Kuboresha na kuimarisha uhifadhi na utunzaji wa rasilimali Misitu, Kutoa ajira za mkataba kwa watoa huduma wa Afya katika Zahanati za Vijiji na Walimu.



*Mifugo*



*Misitu ya Asili H/W ya Tanganyika*

## Miradi ya Umwagiliaji

Tume ya Taifa ya Umwagiliaji inatekeleza Ukarabati wa Skimu ya Mwamkulu na Kabage ambayo inagharimu kiasi cha shilingi **54,686,490,435.28**, Mradi huu ni moja kati ya miradi mikubwa ya kimkakati inayotekelezwa nchini kwa fedha zinazotolewa na Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan Rais wa Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania, fedha zinazotengwa kukarabati miradi ya Umwagiliaji nchini. Aidha ukarabati wa mradi wa Mwamkulu umefika asilimia 22.5 ya utekelezaji na Mkandarasi amelipwa malipo ya awali kiasi cha shilingi **2,743,439,112.00.** Lengo la mradi huu ni kuongeza uzalishaji kutoka gunia 10 za Mpunga kwa ekari moja hadi kufikia wastani wa gunia 40 za Mpunga kwa ekari moja, kulima kwa misimu miwili hadi mitatu, kuongeza eneo la umwagiliaji kutoka hekta **2,700** hadi hekta 6,000 na kuongeza idadi ya wanufaika kutoka Wakulima **600** hadi wakulima zaidi ya **2,400** mradi utakapokamilika.





# 13. MIRADI YA KIMKAKATI

Miradi ya kimkakati iliyotekelezwa ni pamoja na:-

• Barabara ya Mpanda – Tabora km 337,

• Barabara ya Mpanda – Vikonge Kilometa 39.5 imekamilika na inatumika,

• Barabara ya Mpanda – Sitalike km 37 imekamilika na inatumika,

• Barabara ya Vikonge – Luhafwe km 25 ujenzi unaendelea,

• Barabara ya Kibaoni – Sitalike km 50 bado kukamilika ujenzi unaendelea,

• Barabara ya Luhafwe – Mishamo km 37.35 ujenzi unaendelea,

• Daraja la Kavuu urefu Mita 84 ujenzi unaendelea

• Daraja la Msadya urefu Mita 60 limekamilka,
• Shule ya Kanda ya Wavulana Bilioni 4.1 zimepokelewa,

• Shule Maalumu ya Wasichana iliyopo Halmashauri ya Nsimbo zaidi ya Bilioni 4,

Shule mpya 129 (Sekondari 32 na Msingi 97) zimejengwa katika program mbalimbali kama BOOST, UVIKO, SEQUIP, GPE, LANES, P4R, Serikali Kuu, Halmashauri,

• Mradi wa Maji wa Miji 28 katika Manispaa ya Mpanda,

• Ofisi za Umma (Ofisi ya Mkuu wa Mkoa, Ofisi 4 za Wakurugenzi Watendaji wa Halmashauri, Ofisi za Tarafa, Polisi, Zimamoto, Mahakama jumuishi, Mwendesha Mashtaka, CAG, uwanja wa ndege),

• Miradi ya Afya 22 mipya (Hospitali ya Rufaa 1, Hospitali za Halmashauri 4 – Ukarabati 1, Vituo vya Afya na Zahanati 17),

• Mradi wa REA III (II), Vijiji 58 umekamilika na Umeme unawaka kwenye Vijiji vyote 172. pia vitongoji 75 vipo kwenye mpango wa utekelezaji wa mwaka 2024/25 vitafikishiwa huduma ya Umeme,

• Mradi wa Gridi ya Taifa msongo wa 132 kv,

Bandari ya Karema imekamilika na inatumika,

• Miradi ya umwagiliaji Mwamkulu na Kabage imeanza kutekelezwa,

• Miradi takribani 200 kwa fedha zinazotokana na biashara ya Carbon,

• Ujenzi wa vyuo vya VETA 2 (Tanganyika na Mlele) kazi inaendelea,

• Ujenzi wa Ghala, Vihenge na ofisi kwa Taasisi ya NFRA na

• Ukarabati wa reli (Kaliuwa -Mpanda) kilomita 210

• Miradi hii imetatua kero na kuongeza upatikanaji wa huduma kwa jamii.

# MATUKIO KATIKA PICHA



*Rais wa JMT, Mhe. Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan akimjulia hali mgonjwa katika Hospitali ya Rufaa ya Mkoa Katavi.*



*Kamati ya kudumu ya bunge ya TAMISEMI ilipokagua mradi wa ujenzi shule ya sekondari ya wavulana katavi.*



*Mkuu wa Mkoa wa Katavi Mhe. Mwanamvua Mrindoko akishuhudia uwekaji saini mkataba wa ujenzi wa majengo ya Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo, Kampasi ya Mizengo Pinda, Katavi kupitia mradi wa HEET*



*Ziara ya Mkuu wa Mkoa wa Katavi Mhe. Mwanamvua Mrindoko katika mradi wa Maji wa Miji 28 uliopo Kata ya Shanwe Manispaa ya Mpanda.*

# MATUKIO KATIKA PICHA



*Mkuu wa Mkoa wa Katavi Mhe. Mwanamvua Mrindoko akikagua Mradi wa Wodi ya Wazazi na Jengo la Upasuaji Kituo cha Afya Kazima*



*Mkuu wa Mkoa wa Katavi, Mhe. Mwanamvua Mrindoko, akipokea maelezo kuhusu mradi wa Bwawa la Majitaka lililopo katika Kijiji cha Mtakumbuka, Manispaa ya Mpanda.*



*Mkuu wa Mkoa wa Katavi Mhe. Mwanamvua Mrindoko akishuhudia uwekaji saini mkataba wa ujenzi wa miundombinu bwawa la maji - Nsekwa.*



*Ziara ya Mkuu wa Mkoa wa Katavi Mhe. Mwanamvua Mrindoko katika mradi Shule ya Sekondari ya Wavulana Katavi.*